

**CONCOURS EXTERNE ET INTERNE POUR L'ACCÈS A L'EMPLOI DE
SECRETARE DES AFFAIRES ETRANGÈRES
(CADRE D'ORIENT)
AU TITRE DE L'ANNÉE 2023**

ÉPREUVES ÉCRITES D'ADMISSIBILITÉ

Jeudi 22 septembre 2022

SWAHILI

Durée totale de l'épreuve : 3 heures

Coefficient : 2

Toute note globale inférieure à 10 sur 20 est éliminatoire

Dictionnaire autorisé

Barème de notation : composition en swahili 12 points ; traduction en français 8 points



COMPOSITION EN SWAHILI

*Composition en swahili à partir d'une question,
rédigée dans cette même langue, liée à l'actualité
(350 mots avec une tolérance de plus ou moins 10%)*

SUJET :

Je, mahusiano kati ya Urusi na nchi za Afrika ni kitisho au chanzo cha maendeleo kwa bara la Afrika?

**CONCOURS EXTERNE ET INTERNE POUR L'ACCÈS A L'EMPLOI DE
SECRETARE DES AFFAIRES ETRANGÈRES
(CADRE D'ORIENT)
AU TITRE DE L'ANNÉE 2023**

ÉPREUVES ÉCRITES D'ADMISSIBILITÉ

Jeudi 22 septembre 2022

SWAHILI

Durée totale de l'épreuve : 3 heures

Coefficient : 2

Toute note globale inférieure à 10 sur 20 est éliminatoire

Dictionnaire autorisé

Barème de notation : composition en swahili 12 points ; traduction en français 8 points



TRADUCTION EN FRANÇAIS

Traduction en français d'un texte rédigé en swahili

TEXTE AU VERSO

Deutsche Welle, 01/06/2022

Rwanda yasema iko tayari kulipiza kisasi iwapo Congo itashambulia tena

Kiza kikiendelea kutanda katika mahusiano ya kidiplomasia kati ya Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Rwanda imesema haitaki kuvutwa kwenye vita lakini haitaendelea kuvumilia uchokozi wa kurushiwa mabomu na DRC

Waziri wa Mambo ya Nje wa Rwanda, Dkt Vincent Biruta amelilaumu jeshi la MONUSCO la Umoja wa Mataifa kwa kufumbia macho uchokozi huo huku likishirikiana na waasi wa FDLR wenye itikadi za mauaji ya kimbari na lengo la kuipindua serikali ya Rwanda. Akizungumza na waandishi habari mjini Kigali, Waziri wa Mambo ya Nje wa Rwanda Dr Vincent Biruta amesema Jeshi la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo lilirusha mabomu nchini Rwanda tarehe 19 na 23 mwezi jana, lakini Congo haijaomba msamaha. [...]

Rwanda imesema endapo Congo itaendeleza uchokozi wake na kukataa kuwaachia wanajeshi wawili wa Rwanda inaowashikilia ambao Congo inasema walikamatwa wakiwa wameivamia huku Rwanda ikisema walitekwa nyara wakati wakishika doria mpakani, Rwanda itajibu mapigo. [...]

Katika kutafuta suluhisho la amani katika mgogoro huu, rais wa umoja wa nchi za eneo la maziwa makuu ICGLR, Joao Laurengo ambaye pia ni Rais wa Angola jana alifanya mazungumzo na Rais Etienne Tshisekedi wa Congo na anatarajiwa kuzungumza pia na Rais wa Rwanda Paul Kagame.

*

ParsToday, 17/06/2022

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo yasitisha mikataba yote baina yake na Rwanda

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo imetangaza kusitisha mikataba yote iliyotiliana saini na jirani yake Rwanda baada ya kuongezeka mzozo na mvutano baina ya mataifa haya mawili jirani. Baraza la Ulinzi la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo lilikutana jana katika mji mkuu Kinshasa chini ya uwenyekiti wa Rais Felix Tshisekedi ambapo ajenda kuu ilikuwa ni hali ya usalama mashariki mwa nchi hiyo.

Kulingana na msemaji wa serikali ya Kinshasa mikataba yote na makubaliano ya awali iliyotiwa saini na taifa la Rwanda imesitishwa. Rwanda imetakiwa pia kuondoa wanajeshi wake katika ardhi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Jeshi la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo limedai kuwa Rwanda imetuma mamia ya askari ndani ya ardhi ya nchi hiyo, huku wasiwasi na taharuki ikiendelea kushuhudiwa kati ya nchi hizo jirani na kutishia uhusiano baina yao.

Mgogoro wa kidiplomasia baina ya Kigali na Kinshasa umeongezeka katika siku za hivi karibuni baada ya pande zote mbili kutuhumiana kuwa zinaunga mkono waasi mashariki mwa eneo la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo linalopakana na Rwanda.

Serikali ya Kinshasa inaituhumu Kigali kuwa inawaunga mkono waasi wa Kitutsi wa M23 ambao wamekuwa wakitekeleza mauaji ya kinyama huko mashariki mwa DRC.

Katika upande wa pili Rwanda inaituhumu DRC kuwa inawaunga mkono waasi wa Kihutu wa FDLR. Nchi zote mbili zimekanusha madai ya kuwaunga mkono waasi.